# Haki za Maeneo ya Chepechepe




**Maeneo ya Chepechepe, kama Maumbile, huwa na haki ya kuwepo na kustawi, katika hali ya kutenda kazi kamili.**

**Haki za Maumbile[1]:**

| | | |
|---|---|---|
| Maumbile yana haki, sawa na binadamu walivyo na haki | Maumbile yako na haki zake za ya kuwepo, kuwa na mahali ya kuwepo, kustawi/kushamiri, na kuweza kujiendeleza upya na kushiriki katika michakato ya Ardhi | Maumbile yako na haki zake zenyewe, siyo kuwanufaisha watu pekee |

## Kubadilisha Uhusiano Wetu na Maeneo ya Chepechepe

Dhana ya Haki za Maumbile hubadilisha uhusiano wa mwanadamu namaeneo chepechepe kutoka uhusiano wa sasa wa kutumiwa vibaya, kuondoa manufaa, na kumaliza mpaka kuibadilisha kuwa uhusiano unaofahamu haki na uhai wa maeneo chepechepe na hivyo kuanzisha uhusiano uliyo na msingi wausawa, ujamaa, na shukrani na kupangia siku zijazo zenye afya, endelevu na unaolinganisha utawala na ukweli wa kimazingira na tabia nchi.

> “Mabadiliko katika sehemu zote za jamii na uchumi wetu unahitajika ili kuimarisha tabia nchi yetu, kusimamisha upotevu wa bayoanuwai na kupanga barabara inayotupeleka kwa muda ujao tunayotaka.”
>
> Mwenyekiti wa Jopo la Kati ya Maserikali kuhusu Bayoanuwai na Huduma za Mazingira (IPBES) Ana Maria Hernandez Salgar, 2021


**Maendeleo endelevu ya kiikologia huhitaji[2]:**

- Kuishi katika ulinganifu na Maumbile badala ya kuitumia na kuitawala tu
- Wanadamu ni sehemu ya Maumbile, na siyo kando na bora
- Uthabiti wa kanuni za kisheria zinazotawala namna mazingira asili hufanya kazi (mfano “Kushughulika na hali halisi, au sivyo itakushughulikia”)



**Ili kujifunza zaidi: www.rightsofwetlands.org**

**Tamko la Ulimwengu Wote wa Haki za Maeneo Chepechepe[3]**





## Haki ya...

1. Kuwepo.
2. Eneo yao iliyopangwa kimazingira katika ardhi.
3. Mifumo ya kihaidrolojia ya kiasili, yanayoungana, na endelevu.
4. Hali za tabia nchi zinazoweza kuendelezwa kimazingira.
5. Kuwa na maumbile yanayopatikana kiasili, isiyo na aina za maumbile zilizoletwa au zinazovamia na kuharibu ukamilifu wa mazingira.
6. Ukamilifu wa muundo, utendakazi, mchakato wa mageuko ya maumbile, na uwezo wa kutimiza majukumu ya kimazingira katika michakato ya dunia.
7. Kuwa huru kutokana na uchafuzi na uharibifu.
8. Kuzalisha upya na urejesho.


DARWIN INITIATIVE · Wetlands INTERNATIONAL · cobracollective we empower communities · CELDF COMMUNITY ENVIRONMENTAL LEGAL DEFENSE FUND · BSC GROUP · IWMI International Water Management Institute

**Haki za Maumbile ni yenye kuleta mabadiliko kwa sababu hupanga jamii za binadamu ndani ya mazingira.**

**Maendeleo ya Sasa Yenye Uendelevu[4]**




**Haki za Maumbile[5]**




## Ujumbe Muhimu

- Kufanikiwa na ustawi na uendelevu wa maisha Duniani inahitaji mabadiliko ya haraka na yaliyo na matokeo.
- Kutambua, kutekeleza, na kuhakikisha Haki za Maeneo Chepechepe ni mabadiliko muhimu sana katika kupanga shughuli za binadamu na uhakika ya kimazingira.
- Wanadamu wana jukumu la kimaadili ya kutambua Haki za Maumbile, ikiwemo Haki za Maeneo Chepechepe na vipengele vya Maumbile kuishi, na kuwa na mahali pa kuwa, na kushiriki kikamilifu katika Mtandao wa Maisha.

### Maeneo Chepechepe yenye afya hayawezi kuwepo bila haki zote 8.

- Watu wa Kiasili na Jamii za Eneo ndiyo viongozi katika kutambua Haki na uhai wa Maumbile na jukumu na wajibu wa binadamu kama washiriki katika utandu wa Maisha.
- Mifumo ya kisheria ya kutekeleza Haki za Maumbile zipo, na hutumika kwa Haki za Maeneo Chepechepe.
- Jamii husika zenyewe pia wanaweza kuchukua, na tayari wanachukua hatua ili kubadilisha uhusiano wao na maeneo chepechepe.
- Haki za Maeneo Chepechepe huweza kukuzwa na kutegemezwa kupitia mikakati ya kitamaduni, kielimu, kisheria, kusimamia maeneo chepechepe.

## Mbona Sasa?

**Tuko katika njia panda. ijapokuwa zipo juhudi za kulinda maeneo chepechepe na kuzirudisha upya, bado kuna upotevu na uharibifu wa maeneo chepechepe zinazoendelea, huku ikiwa na asilimia 35% ya maeneo chepechepe[6] ulimwenguni yakiwa yamepotea tangu miaka ya 1970[7,8].**

Upotevu na uharibifu wa Maeneo Chepechepe huchangia mabadiliko katika tabia nchi na uharibifu na upotevu katika maumbile tofauti. Taratibu zilizopo za ulinzi, kurudisha upya, na maendeleo endelevu yameshindwa kubadilisha uhusiano wa binadamu-na Maumbile au kusimamisha tabia ya binadamu inayofuata matumizi na ambayo imetufikisha kwenye ukingo wa uharibifu wenye maafa wa tabia nchi na ambayo umeleta kutoweka kwa uhai mkubwa wa 6, yote ambayo inafanyika haraka zaidi ya kiasi iliyotarajiwa. Tuna muda mchache uliosalia kubadilisha mwelekeo, kwa hivyo lazima tuchukue hatua sasa.

## Jinsi Ya Kuendelea

Kwa milenia nyingi na katika tamaduni tofauti, watu wametambua Haki za Maumbile na vipengele vya Maumbile kama washirika katika Mtandao wa Maisha[9]. Kutofautishwa kwa binadamu kutoka Maumbile mengine na kuwaweka wanadamu juu ya Maumbile umesababisha hali za dharura za sasa za maeneo chepechepe, maumbile tofauti, na katika tabia nchi, ikiwa ni matumizi yenye uharibifu na ya matumizi zaidi ya maeneo chepechepe na vipengele vingine vya Maumbile yakileta hali hizi za dharura. Vinginevyo, wakati wanadamu wanafahamiwa kuwa sehemu ya Maumbile, huku maeneo chepechepe na Maumbile ina Haki, basi uhusiano wa mwanadamu-Maumbile itakuwa yenye msingi wa kulipia, shukrani, na mizani, ikiwamo wajibu wa kimaadili ambazo watu wanao kwa Maumbile, kama vile Watu wengi wa Kiasili na Jamii husika (IPLC) hudhihirisha na wamedhihirisha kwa muda wote.

1,2,4,5 Kauffman, C. M. & Martin, P.L. 2021. *The Politics of Rights of Nature: Strategies for Building a More Sustainable Future.* MIT Press. Cambridge, MA.

3 Davies GT, Finlayson CM, Pritchard DE, Davidson NC, Gardner RC, Moomaw WM, Okuno E, Whitacre JC, 2020. Towards a Universal Declaration of the Rights of Wetlands. Marine and Freshwater Research. https://doi.org/10.1071/MF20219

6 Including both inland/freshwater and coastal/saltwater wetlands.

7 Ramsar Convention on Wetlands, 2018. *Global Wetland Outlook: State of the World's Wetlands and their Services to People.* Gland, Switzerland: Ramsar Convention Secretariat.

8 Where data is available.

9 Supplementary material in Davies GT, Finlayson CM, Pritchard DE, Davidson NC, Gardner RC, Moomaw WR, Okuno E, and Whitacre JC. 2020. Towards a Universal Declaration of the Rights of Wetlands. *Marine and Freshwater Research* 72(5) 593-600. https://doi. org/10.1071/MF20219